



Kudhihirisha Teknolojia za KCSAP, Ubunifu na Usimamizi Bora katika Ufugaji wa Nyuki

Na DKT REMY TUEY NA DKT JANE WAMUONGO

Ufugaji wa nyuki ni aina ya kilimo kilichokita mizizi sana nchini Kenya na kinaweza kufanikishwa katika takribani asilimia 80 ya maeneo ya nchi hii. Kinastahili hasa katika maeneo kame ambapo kilimo kinachotegemea mvua hakifaulu kwa urahisi.

Ufugaji wa nyuki hutekeleza jukumu muhimu katika kufanikisha utoshlevu wa chakula, ustawi wa uchumi, uhifadhi wa viembe-hai na riziki kupitia kwa kuzalisha asali, nta ya nyuki/masega ya asali, utomvu na uchavushaji wa mimea. Uwezo wa uzalishaji katika sekta ya ufugaji nyuki nchini unakadiriwa kuwa zaidi ya tani 100,000 za asali na tani 10,000 za nta za nyuki kwa mwaka.

Lakini licha ya uwezo mkubwa wa sekta hii ya ufugaji nyuki, juhudi ndogo sana zimefanaya kuivumisha sekta hii. Zipo changamoto ambazo iwapo zitashughulikiwa, zinaweza kuimarisha sana sekta hii. Changamoto hizo zinahusu aina ya mizinga katika eneo fulani, magonjwa/Wanyama waharibifu katika eneo husika, nini kinachangia nyuki kukwepa au kutoroka mizingani, uwepo wa malisho ya nyuki miongoni mwa nyingine.

Usimamizi bora wa mizinga ya nyuki pamoja na ubunifu vinaweza kutoa jibu mwafaka na kupunguza nyuki kususia mizinga mbali na kuongeza kiwango cha uzalishaji.

Uharibifu wa mazingira-asili ambayo ni makazi ya nyuki, pamoja na uhaba wa utafiti wa teknolojia za kufuga nyuki, ukosefu wa maarifa tosha ya kusimamia nyuki na kiwango duni cha uzalishaji kutokana na urinaji mbovu na uchavushaji wa asali ni miongoni mwa changamoto hizo. Mizinga ifuatayo inaweza kusaidia kupunguza tatizo la uzalishaji mbovu:



Asali iliyotayarishwa na kupakiwa kwenye makopo kwa mauzo bora.



Mzinga wa Kapkuiki, Baringo ya Kati.

UIMARISHAJI WA KAPKUIKI WA GOGO IMARA: Huu ni mzinga unaotengenezwa kitamaduni ambapo mafundishungu.

UIMARISHAJI WA PAA LILIOILULIWA: Katika kukabili tatizo la nyuki kukwepa mizinga yenye paa la chuma, ya KTBH, kutokana na kiwango cha juu cha joto, mizinga maalum ya KTBH imeundwa ambayo paa lake liko juu zaidi.

UIMARISHAJI WA KISANDUKU ULIOIMARISHWA:

Ubunifu wa mzinga wenye paa la kuingiza hewa pamoja na kupunguza joto umefaulu zaidi. Mzinga huu umevumishwa hasa Kiambu, Isiolo, Siaya na Kitui japo haujakumbatiwa sana.

Njia nyingine faafa za kuimarisha uzalishaji asali

Mtindo bora wa kufuga nyuki
Hii inahusu mbinu ya kiusimamizi ambayo ilibuniwa ili kukiuka changamoto za uzalishaji duni, usimamishaji usio sahihi wa mizinga na utorokaji wa nyuki katika mizinga.

Urinaji bora wa asali, utunzaji na utayarishaji bora wa asali iliyorinwa

Malisho jumuishi ya nyuki:
Huu ni mtindo uliobuniwa kuondoa changamoto ya kuharibwa kwa maskani ya nyuki hasa kutokana na ulishaji mifugo uliopita kiasi na uharibifu wa kibinadamu.

Waadishi wa makala haya ni wanasayansi wa shirika la KALRO chini ya ufadhili wa shirika la KCSAP katika ushirikiano unaoitwa Collaborative Research Grants.

“
Usimamizi
bora wa
mizinga
ya nyuki
pamoja na
ubunifu
vinaweza
kutoa jibu
mwafaka...”